

GRADE 5 MID TERM 2 MAY 2022

ANSWER SHEET

TARGETER WINGS

KUTATHMINI HATUA YA MWANAFUNZI

GREDI 5 - 2022

KISWAHILI : INSHA



Jina: .....

Jina la shule: .....

Viwango vya kutathmini				
	Kuzidisha matarajio	Kufikia matarajio	Kukaribia matarajio	Mbali na matarajio
Kuandika	9 - 10	6 - 8	3 - 5	0 - 2

**Kuandika (Alama 10)**

**Andika insha kuhusu:**

**WANYAMA WA PORINI**

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

# TARGETER WINGS

## KUTATHMINI HATUA YA MWANAFUNZI

### GREDI 5 - 2022

## SHUGHULI ZA KISWAHILI



Jina .....

Jina la shule .....

Mwalimu ajaze mjalizo baada ya kusahihisha kazi ya mwanafunzi.

Viwango vya kutathmini				
	Kuzidisha matarajio	Kufikia matarajio	Kukaribia matarajio	Mbali na matarajio
Kusikiliza na Kuzungumza	5 <input type="checkbox"/>	4 <input type="checkbox"/>	3 <input type="checkbox"/>	0 - 2 <input type="checkbox"/>
Kusoma kwa sauti	Maneno 61 na zaidi <input type="checkbox"/>	Maneno 51-60 <input type="checkbox"/>	Maneno 25 - 50 <input type="checkbox"/>	Maneno 0 - 24 <input type="checkbox"/>
Sarufi	19 - 20 <input type="checkbox"/>	13 - 18 <input type="checkbox"/>	6 - 12 <input type="checkbox"/>	0 - 5 <input type="checkbox"/>
Ufahamu	5 <input type="checkbox"/>	4 <input type="checkbox"/>	3 <input type="checkbox"/>	0 - 2 <input type="checkbox"/>

### I. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

Jibu maamkizi na maagano yafuatayo

- Maagano** **Majibu**
  - Kwa heri  \_\_\_\_\_
  - Lala unono  \_\_\_\_\_
- Maamkuzi** **Majibu**
  - Hujambo  \_\_\_\_\_
  - Alamsiki  \_\_\_\_\_
  - Sabalheri  \_\_\_\_\_

## II. KUSOMA KWA SAUTI:

### Soma kifungu hiki kwa sauti

Sijali alionywa mara nyingi dhidi ya tabia yake ya kuandamana na genge la wezi. Yeye hakusikia la mwadhini wala la mteka maji msikitini. Maneno ya wavyele wake aliyapa kisogo. Alitia masikio nta.

Jioni moja alitoka kama ilivyo desturi yake: Hakutaka ijulikane alikoelekea. Aliandamana na wenzake kama kawaida. Waliandamana hadi kwa bwanyenye fulani kuiba. Kumbe siku zake arubaini zilikuwa zimetimia. Kutokana na kupuuzwa kwake alifyatuliwa risasi na kufa papo hapo.

## III. UFAHAMU: (Alama 10)

### Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Mwajuma alikuwa na kipawa cha kipekee. Alikuwa ametunukiwa sauti ya kuvutia. Alikuwa na sauti nzuri kama kinanda. Nao walimu walikitambua kipawa hicho na kumhimiza akjendeleze. Alianza kwa kukariri mashairi yenye mishororo minne yaani tarbia. Hatimaye alijiunga na kwaya na kuteuliwa kama ngoi wa kuongoza kwaya hiyo. Aliheshimiwa sana ingawa hakujimudu katika masomo. Kweli 'mguu mtembezi haukosi mwiba!'

a) Taja kipawa alichokuwa nacho mhusika \_\_\_\_\_ (alama 1)

b) Ni kina nani walikitambua kipawa chake Mwajuma? \_\_\_\_\_ (alama 1)

c) Kulingana na aya ya pili, mashairi yenye mishororo minne huitwaje? \_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_ (alama 1)

- d) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika kifungu hiki. (alama 1)
- i) Kuvutia \_\_\_\_\_
- ii) Ngoi \_\_\_\_\_
- e) 'Mguu mtembezi haukosi mwiba' ni mfano wa tamathali ipi ya lugha? (alama 1)
- \_\_\_\_\_
- f) Je, walimu wake Mwajuma walimhimiza afanye nini? (alama 1)
- \_\_\_\_\_
- g) Tambua tashbihi iliyotumika katika kifungu? (alama 1)
- \_\_\_\_\_

**IV. SARUFI (Alama 20)**

**Jibu kulingana na maagizo.**

1. Andika kinyume cha maneno yafuatayo (alama 5)

<u>Kitenzi</u>	<u>Kinyume</u>
a) bandika	_____
b) malkia	_____
c) keti	_____
d) mgeni	_____
e) giza	_____

2. Tunga sentensi mbili kuonyesha maana ya maneno uliyopewa. (alama 2)

- a) shaba \_\_\_\_\_
- b) shamba \_\_\_\_\_

3. **Kamilisha methali zifuatazo.**

(Alama 3)

- a) Asiyekuwapo na \_\_\_\_\_
- b) Kikulacho \_\_\_\_\_
- c) Aisifuye mvua \_\_\_\_\_

4. **Kamilisha tashbihi zifuatazo.**

(alama 4)

- a) Fatuma ana maringo kama \_\_\_\_\_
- b) Yeye ni mweusi kama \_\_\_\_\_
- c) Pahali papo palikuwa baridi kama \_\_\_\_\_
- d) Alizaa mtoto mrembo kama \_\_\_\_\_

5. **Andika vitenzi vifuatavyo katika kauli ya kutendwa.**

(alama 5)

**Kitenzi**

- a) Cheza \_\_\_\_\_
- b) Lima \_\_\_\_\_
- c) Lia \_\_\_\_\_
- d) Anika \_\_\_\_\_
- e) Ruka \_\_\_\_\_

6. Taja sehemu moja ya mwili inayopatikana kichwani.

(alama 1)

\_\_\_\_\_